Learning on TAP

# Upimaji wa uoni na usikivu kwa watoto wa umri wa shule

## Maneno Muhimu: Utangulizi wa upimaji wa milango ya fahamu (sensory screening

| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Kifaa saidizi** | Vifaa saidizi ni vifaa vinavyotumiwa na watu kuweza kufanya kazi ambazo wasingeweza kuzifanya vizuri au kutokuzifanya kabisa iwapo wasingekuwa na vifaa hivyo | |
| **Audiomita** | Kifaa cha kupima usikivu |  |
| **Brele** | Ni aina ya lugha kwa watu wasioona. Herufi zimewakilishwa na vidoti doti vilivyo kwenye mpango maalum. Waweza kuhisi vidoti hivi kupitia kwenye ncha za vidole. | |
| **Kifaa saidizi cha usikivu** | Kifaa hiki kinavaliwa kwenye sikio na watu ambao wanapata changamoto ya kusikia. Kifaa saidizi cha kusikia kinaongeza ukubwa wa sauti kiasi kwamba mtu mwenye changamoto ya kusikia anaweza kusikia, kuwasiliana na kushiriki kikamilifu shughuli za kila siku. |  |
| **Otoskopu** | Kifaa cha kuongeza ukubwa kwa kutumia mwanga unaotumika kukagua sikio la mtu anayefanyiwa kipimo |  |
| **Mfanyakazi** | Mtu anayefanya kazi kwenye utoaji huduma au shirika. Hii inajumuisha watu ambao walipata mafunzo kwenye eneo maalumu la afya ambao yawezekana hawana vigezo vya kitaaluma | |
| **Mpimaji** | Mtu anayefanya kipimo | |
| **Upimaji wa milango ya fahamu** | Ni mchakato wa kuangalia macho na masikio ya mhusika kama yana afya na kuainisha matatizo kwenye kuona na kusikia | |